# KISWAHILI KIDATO CHA KWANZA

# MTIHANI WA MUHULA WA KWANZA 2024

**MWONGOZO**

**Ufahamu**

(a) HATARI ZA UGONJWA WA UKIMWI/UKIMWI (Alama 1)
maneno yasizidi 6.

(b) kukonda sana kwa waathiriwa.
Awali waliofariki kutokana na ukimwi hawakuwa wakizikwa na jamaa zao.
(2 x 1 = 2)

(c) - Awali watu waliwaona wagonjwa hao kama waasi au wahalifu waliojiletea balaa.
- Walistahili kuepukwa kabisa kwa hofu ya kuambukiza wengine viini vya maradhi ya ukimwi. (Alama 2)

(d) – Kuhusika katika ngono na mtu aliyeambukizwa virusi vya ukimwi.
- Athari ya kuwa na wapenzi wengine.
- Matumizi ya vifaa vyenye makali na watu wenye virusi vya ukimwi.
- Mama mtu anaweza kusambaza virusi kwa mtoto wake wakati wanapojifungua na kumnyonyesha.
- Mtu anapotiwa damu yenye virusi vya ukimwi huambukizwa mara moja.
(Alama 3 x 1 = 3)

(e) – Kutofanya mapenzi kiholela bila kutumia kinga yoyote.
- Kutoshirikiana na watu wanaougua ugonjwa huu katika matumizi ya vifaa vyenye makali.
- Kuwa waaminifu na kumcha Mungu.

(Alama 2 x 1 = 2)

(f) kuimarisha kinga ya magonjwa katika mwili wako

(g)
i) Uwele – Ugonjwa, maradhi
(ii) Haujafua dafu- haujafaulu/haujafanikiwa
(iii) kuenda jongomeo- kufariki/kufa/kupoteza uhai

(alama 3x 1 = 3)

**2. MATUMIZI YA LUGHA.** **(ALAMA 40)**

a) Sauti

Silabi



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

Neno

Sentensi (4x1=4)

b) i) konsonanti

irabu/vokali (2x1= 2)

ii) Konsonanti zinapotamkwa hewa hubanwa/huzuiliwa katika ala za kutamkia mf /z/ ilhali irabu hutamkwa kwa ulaini/ bila kubanwa kwa hewa katika ala za kutamkia.mf /a/

(2x1=2)

c)

/a/; irabu ya chini na kati. Hutamkwa midomo ikitandazwa

/o/ irabi ya kati na nyuma. Hutamkwa midomo ikiviringwa

Alama 6 x ½= 3)

d)

i. Vipasuo/ sauti za mtuo:/p/, /b/, /g/, /k/, /d/, /t/, /j/
ii. Vikwamizo/Vikwaruzo: /f/, /v/, /s/, /sh/, /th/, /dh/, /z/, /h/, /gh/
iii. Kipasuo kwamizo/kwaruzo:/ch/
iv. Nazali/Ving'ong'o/vipua:/m/,/ng'/,/ny/,/n/
v. Kitambaza:/l/
vi. Kimadende: /r/
vii. Nusu irabu/Viyeyusho:/w/,/y/

(7x1=7)

e)

Ala tuli ni ala za sauti zisizosonga wakati wa utamkaji mf ufizi ilhali ala sogezi ni ala zinazosonga wakati wa utamkaji mf ulimi. 2x1=2

f) i. pigo la sauti katika neno (1x1=1)

ii. M-funge kwani inaishia K

tu- wazi kwani inaishia I 2x1=2

iii. KKKI-KI mbweha, ngwena n.k (1x1=1)

g)

**Ba'rabara** wanafunzi wapenzi wa Kiswahili **bara'bara** zote zinaelekea mjini kwa tamasha za muziki. (2x1=2)

h)

Kiziwi; A-WA

Karatasi; I-ZI



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Meza; I-ZI 3X1=3

i)

Lo!Mwizi sugu sana na mwenzake walikamatwa na askari ndani ya msitu

Lo! kihisishi

Mwizi/askari/msitu; nomino

Sugu; kivumishi

Sana; kielezi

na; kiunganishi

mwenzake; kiwakilishi

walikamatwa; kitenzi

na/ ndani ya; kihusishi

8 x ½= 4

j)

Wakulima bora hupokea mazao tele kutoka mashambani 2x1=2

k)

Hutasoma vizuri sana 1x2=2

l) Karimu ni kwa -choyo, tua ni kwa **twika** (alama 1)

m) KN; wanfunzi wote wenye bidi

KT; watapita mtihani huu.

(2x1=2)

**3. ISIMUJAMII (ALAMA 10)**

1.

Isimu; somo / taaluma inayochunguza lugha kisayansi



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Jamii; watu wanaoishi Pamoja na wenye utamaduni mmoja

Isimujamii; somo linalochunguza uhusiano wa lugha na jamii

Lugha; mfumo wa sauti nasibu na ishara zinazofanikisha mawasiliano

4x1=4

2. Chombo cha mawasiliano

Chombo cha ajira

Kuburudisha

Kitambulisho cha mtu na utamaduni wake.

Kuendeleza elimu

Kuendeleza dini

Serikali kupitisha sera zake

Eleza zozote (6x1=6)

Kadiria 7x1=7

**4. FASIHI SIMULIZI (ALAMA 15)**

a)

i) Fasihi; sana ya lugha kuhusu binadamu.

j) Sanaa;ufundi wa kuwasilisha fikra na hisia za binadamukama vile maneno, maandishi, uchoraji.

ii) fasihi simulizi; Sanaa ya lugha inayopitishwa kwa masimulizi/mdomo

iii) fasihi andishi; Sanaa ya lugha inayopitisha ujumbe kwa maandishi.

(4x1=4)

b) Fasihi ina umuhimu gani katika jamii? (alama 6)

i. Kuburudisha/kustarehesha/kufurahisha/ kuchangamsha/kusisimua na kupumbaza akili na kiwiliwili – ujumbe huwasilishwa kwa njia ya kuvutia na kuleta ucheshi
ii. Kuadilisha /kufunza maadili kwa wanajamii kwa kuwahimiza kuiga sifa chanya na kukataa sifa hasi za wahusika.
iii. Kukuza uwezo wa kufikiri/kudadisi k.m vitendawili na chemshabongo.
iv. Vipengele vya fasihi simulizi k.v mashairi, nyimbo, nahau, hutumiwa katika uandishi wa fasihi andishi.
v. Kuhifadhi historia ya jamii k.m. mighani, visaviini, mapisi, tarihi n.k. hizi hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
vi. Kukejeli tabia zinazokiuka matarajio ya jamii k.v soga, methali, n.k.
vii. Kuendeleza tamaduni za jamii kwani husawiri imani na desturi za jamii. k.v kitendawili ‘Nyumbani mwetu mna papai lililoiva lakini siwezi kulichuma.’ - Mtu hawezi kumwoa dadake.
viii. Kuunganisha watu pamoja kwa kuwajumuisha pamoja wakati wa ngoma, kuimba, utambaji, n.k.


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

ix. Kukuza lugha k.v. ulumbi na misimu inapokita kimatumizi na kujumuishwa katika lugha sanifu.
x. Kukuza ubunifu k.v. malumbano ya utani, vitanza, ndimi ngonjera, n.k.
xi. Kukuza uzalendo kwa kufanya wanajamii kuonea fahari jamii zao na kuiga mashujaa au watu waliotendea jamii makuu.
xii. Kuonya na kutahadharisha wanajamii dhidi ya tabia hasi k.v. ulafi, uchoyo, n.

6x1=6

c) Linganisha fasihi simulizi na fasihi andishi (alama 5)

i. Zote mbili hushughulikia masuala yanayohusu maisha maisha ya binadamu.
ii. Zote mbili Hutumia lugha kwa ubunifu kuwasilisha maudhui.
iii. Zote mbili huwa na vipengele viwili vikuu, maudhui na fani (jumla ya mbinu msanii alizotumia kuwasilisha maudhui).
iv. Zote mbili majukumu sawa k.v. kuburudisha, kuadilisha, kuhifadhi na kuendeleza utamaduni, n.k.
v. Zote mbili zina utendaji-pale tamthilia na riwaya zinapoigizwa.
vi. Zote mbili huzaliwa, hukua na hufa kutegemea mabadiliko ya wakati.
vii. Zote mbili huwa na wawasilishaji-fanani k.m. mtambaji/mganaji au manju/yeli katika fasihi simulizi na mwandishi upande wa fasihi andishi .
viii. Fasihi andishi imekopa vipera vya fasihi simulizi k.v. methali, mashairi, n.k.
ix. Zote mbili zina maudhui na dhamira zinazofanana.

Za kwanza 5x1=5


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes